

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TISA**

**KIKAO CHA TATU**

**03 NOVEMBA, 2022**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TISA

KIKAO CHA TATU – TAREHE 03 NOVEMBA, 2022

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

40. **MHESHIMIWA JACQUELINE ANDREW  
KAINJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza majengo katika Kituo cha Afya Itobo Wilayani Nzega.

41. **MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS  
NDAKIDEMI (MOSHI VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Daraja Kata ya Arusha chini litakalounganisha Vijiji vya Muungano, Mikocheni na Chemchem.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**42. MHESHIMIWA GEOFFREY IDELPHONCE MWAMBE (MASASI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ualimu Masasi baada ya Chuo cha Ualimu Ndwika kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**43. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini TFS itanza kutoa Vibali vya Malisho kwa Wafugaji kama inavyotoa Vibali vya Kuvuna Mbao na Mkaa ili Serikali ipate mapato.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **44. MHESHIMIWA HASSAN HAJI KASSIM (MWANAKWEREKWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mkakati gani wa kuitanua sehemu ya kusafirishia abiria wanaokwenda Zanzibar katika Bandari ya Dar es Salaam.

## **WIZARA YA AFYA:**

### **45. MHESHIMIWA TECLA MOHAMEDI UNGELE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kupeleka Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mifupa katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Lindi.

## **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

### **46. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-


Je, Serikali ina mkakati gani juu ya mashamba makubwa yanayomilikiwa na Wawekezaji na hayatumiki kuzalisha mali na ajira nchini.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**47. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga Minara ya Simu katika Kata za Jimbo la Ludewa pamoja na kuongeza nguvu kwa minara iliyopo iwe 4G.



**WIZARA YA MAJI:**

**48. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini RUWASA Nyasa itapatiwa gari ili kurahisisha utendaji kazi.

#### **IV. HOJA ZA KAMATI:**

##### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):**


Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

##### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA  
BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA  
(PIC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.



***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
03 NOVEMBA, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**